

# Pambazuko

Toleo Namba 0043


Jumatatu Julai 24-30, 2023



Askofu KKKK Karagwe  
Dkt Benson Bagonza



Sheikh Mkuu wa Tanzania  
Abubakar Zubeir bin Ally



Katibu Shura ya Maimam  
Sheikh Issa Ponda

## Hatari ya udini inanyemelea Tanzania

- *Inajificha kwenye fukuto la 'Mkataba wa Bandari'*
- *Mparaganyiko wa Wabara, Wazanzibari wadhihiri*



Mkuu wa KKKK Askofu  
Dkt. Frederick Shoo



Katibu Bakwata Sheikh  
Khamis Mattaka



Rais wa TEC Gervas  
Nyaisonga

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Msimamo

## Tukemee ubadhirifu kwa vitendo

**M**ARA kadhaa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa Kassim Majaliwa, amesikika akifoka, akionekana kukerwa na zaidi sana akithibitika kukasirika kwa matukio anayoyataja kuwa ni ubadhirifu na matumizi mabaya ya ama madaraka au fedha za walipakodi anapokuwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo.

Ikumbukwe kuwa Septemba 8, mwaka jana, Majaliwa akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Tabora, alifika kwenye mradi wa ujenzi wa Chuo cha Veta Uyui, ambako alishangazwa kusikia kuwa kibanda cha mlinzi wa chuo hicho kimegharimu Sh. milioni 11.

Majaliwa alisema kwa muonekano, kibanda kile hakiwezi kuchukua kiasi hicho cha fedha alichoeleza na kwamba huenda kuna ubadhirifu umefanywa na kuamuru Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) kuwakamata na kuanza kuwachunguza wote waliohusika katika mchakato wa ujenzi huo.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa kiongozi huyo mkuu wa shughuli za serikali bungeni na mshauri -mtendaji wa karibu kabisa wa Rais Samia Suluhu Hassan, akifoka na kuamuru watendaji kukamatwa akiwa kwenye kadamasini.

Pamoja na kwamba ni hatua nzuri kwa kiongozi wa juu kuonekana kukwera na yanayoendelea katika utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana, bila kuwaibia wananchi kodi zao, bado

kuna maeneo ambako Rais Samia, Majaliwa na uongozi mzima wa serikali, wameshindwa kuonyesha hasira zao.

Maeneo hayo ni yale yanayothibitika katika vitabu vya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba kuna wizi mkubwa wa fedha za walipakodi wa Tanzania na hata zile zinazoletwa kwa njia ya mikopo na hata misaada kutoka nchi washirika wa maendeleo.

Kila mwaka CAG amekuwa akiibua madudu ya kutisha katika halmashauri, taasisi, wakala, kampuni na hata mashirika yanayoendeshwa na serikali moja kwa moja au kuwa na ubia, lakini hasira na sauti za kufoka hazisikiki kuwa kuu na zenye ukali kwa wahusika wanaoweza kuwekwa kwenye kundi la 'mapapa wezi.'

Pamoja na ubaya wa ubadhirifu mdogo, madhara yake yanaweza kuwa makubwa ikiwa yatajikusanya hata kufikia viwango vya ufisadi, ambao una ubaya mkubwa zaidi na kuwa na madhara yanayoumiza jamii pana zaidi.

Watanania wanapenda kuona serikali ikichukua hatua kali zaidi kwa wote wanaofisidi nchi hii, hasa hao wanaobainika kukwapua fedha za maendeleo kwa manufaa binafsi, huku wakifanya mnyororo wa umasikini kuendelea kuwafunga wengi zaidi – na hata kupokewa na vizazi na vizazi.

Ikiwa hasira za serikali zitabaki kwa "vidagaa" tu, na mafisadi papa kuachwa, basi hata uchunguzi wa CAG na ushauri wake, hautakuwa na maana zaidi ya kujaza karatasi katika kabati za ofisi za wakubwa.

## **MGENI NJOO.....**



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kulia) Samia Suluhu Hassan akizungumza na mgeni wake, Rais wa Hungary, Katalin Novák - Ikulu, jijini Dar es Salaam 18 Julai, 2023. Rais Novák alikuwa nchini Tanzania kwa siara ya siku tatu. (Picha na Ikulu)*

### **Jisajili kupata Pambazuko bure**

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### **NUKUU**



*Rais Samia (Suluhu Hassan) kufanikiwa kufikia leo ni utulivu pekee unamsaidia, maana hakuna nafasi ngumu kama aliyonayo, lakini kwa sababu ya utulivu wake - ingawa ana hasira, lakini mambo yanaenda, hiyo pekee inatosha mimi kujivunia yeye baada ya kumuibua huko Zanzibar na kumleta Muungano - Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete; Julai 18, 2023 Jijini Arusha.*

## Habari

### Mparaganyiko wanyemelea Tanzania

Na Ismail MOHAMMED

**S**ASA ni dhahiri kwamba uimara wa amani, utulivu na kuaminiana miongoni mwa Watanzania, kumetikishwa, Pambazuko linabaini.

Kinachoonekana kutikisa mihimili hiyo – iliyokuwa ikibeba sifa za Tanzania ni mgongano wa mawazo, hoja, usahihi wa takwimu, sheria na hata misimamo ya mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, vyama vya siasa, dini na kada za wasomi na wanazuoni.

Pambazuko limebaini kuwa kinachogonganisha Watanzania sasa, hata kufikia hatua ya kuacha kujadili hoja na kusababisha kutukanana na “kuvunjiana heshima” miongoni mwao, ni uwekezaji wa Kampuni ya DP World ya Dubai katika kuendeleza, kuboresha, kuendesha na kusimamia baadhi ya bandari za Tanzania.

“Wanaonyukana” zaidi kupitia mitandao ya kijamii, mikutano ya ndani na hadhara ni baadhi ya wanasheria, viongozi wa dini, viongozi na wanachama wa vyama vya siasa, waandishi wa habari, wasomi na wananchi wa kada mbalimbali.

Kitovu cha mnyukano huo ni kufungwa kwa makubaliano ya serikali mbili (IGA) za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirati ya Dubai, hasa katika uendeshaji wa bandari za Tanzania.

Dubai ni sehemu mojawapo kati ya Muungano wa Emirati Saba za Kiarabu.

Baada ya kufungwa kwa makubaliano hayo mjini Dodoma, Oktoba 25, 2022, na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Tanzania - Juni 10, 2023, minyukano yenye kutishia umoja wa kitaifa, ikaanza kwa kujikita katika maeneo ya kijiografia, kisiasa, na kidini.

Minyukano ya kijiografia ilianza siku

chache kabla ya Bunge kuidhinisha makubaliano haya, pale Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alipohoji umakini wa makubaliano haya, katika namna ambayo ilionyesha kwamba, anataka kusema kuwa, Tanzania imeingia makubaliano mabaya kwa sababu watu waliosaini makubaliano hayo wanayo asili ya Zanzibar.

Mbowe alitoa maoni yake kwa kuuliza swali lifuatalo: “Kama Makubaliano haya yanayo Manufaa kwa nini yanaibagua Zanzibar?”

Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa hati ya nguvu ya kisheria kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kusaini makubaliano hayo. Sheria za Tanzania zinampa haki rais kufanya hivyo.

Katika suala hili, Mbowe alionekana kusema kwamba, watia saini hawa hawakuwa na uchungu wa mali za Tanzania Bara, kwa kuwa asili yao ni Zanzibar.

Lakini, hoja hii imepingwa na wachangiaji baki kwa sababu ya rai kwamba, ubaya na uzuri wa makubaliano haya unaweza, na unapaswa, kujadiliwa bila kuangalia nani waliyasaini au anayechangia mawazo anatoka upande gani wa Muungano.

Mchango wa Profesa Issa Shivji, mtaalam wa sheria, ambaye anayo asili ya Tanzania Zanzibar, ulithibitisha mtazamo huu.

Minyukano ya kisiasa ilianza kudhihirika Bungeni siku yalipofanyika majadiliano ya kuidhinisha makubaliano haya, Juni 10, 2023.

Wakati wa majadiliano hayo, wabunge wote wa CCM waliochangia waliunga mkono hoja, lakini bila kujielekeza kwenye vifungu vya makubaliano haya. Siku hiyo, waongaji wakuu kutoka

## **Mparaganyiko wanyemelea Tanzania**

kambi ya CCM walikuwa ni Charles Katambi, Prof. Kitila Mkumbo na Leonard Chamuriho

Na kwa upande mwingine, wabunge wote wa kambi ya upinzani walipinga hoja iliyowasilishwa Bungeni. Jitihada zao za kujikita kwenye kujadili maudhui ya makubaliano zilidhoofishwa na heka heka za wabunge wa CCM kutaka kutoa “taarifa” kila baada ya muda mfupi kwa waongejaji kutoka kambi ya upinzani. Siku hiyo, waongejaji wakuu kutoka kambi ya upinzani walikuwa ni Halima Mdee na Aida Kenan.

Lakini baadaye, kadiri mijadala ilivyopamba moto ikadhihirika kwamba, ubaya na uzuri wa makubaliano haya unaweza, na unapaswa, kujadiliwa bila kuangalia anayechangia mawazo anatoka kambi gani ya kisiasa.

Na minyukano ya kidini imebuka baada ya viongozi wa dini kama vile Sheikh Said Mwaipopo kuanza kujenga hoja kwamba wanaokosoa makubaliano haya wanafanya hivyo kwa sababu yanawahusu Waislamu wa Dubai ambao wana undugu wa kidini na Waislamu wa Tanzania.

Kwa maoni ya Shekhe Mwaipopo, kupinga makubaliano haya ni sawa na kupinga Uislamu.

Hata hivyo, mawazo yake yamekosa mashiko baada ya watu kubaini kuwa ubaya na uzuri wa makubaliano haya unaweza, na unapaswa, kujadiliwa bila kuangalia anayechangia mawazo anatoka kambi gani ya kidini. Jambo hili llimethibitishwa na michango ya ukosoaji iliyotolewa na Profesa Issa Shivji, ambaye ni mfuasi wa dini ya Kiislamu.

Askofu Dkt. Benson Bagonza wa KKKT Dayosisi ya Karagwe, anasema kwamba, “wanaolazimisha mjadala kuhusu makubaliano ya Bandari kuendeshwa

kwa kutumia misamiati ya kambi za kijiografia, kisiasa na kidini wanataka kutusahaulisha hoja ya msingi, maana bandari zetu hazina dini wala itikadi ya kisiasa.”

Kwa upande mwingine, Sheikh Maulid Ramadhani wa Mtwara, amesisitiza kwamba, “bandari zetu ndio uzima wa Watanzania wote, bila kujali dini, itikadi ya siasa, wala eneo la makazi ya mtu, maana mahitaji yote muhimu kwa ajili wananchi yanaingia nchini kupitia bandarini.”

Dkt. Anita Mushi, mchambuzi mbobezi wa siasa za kimataifa, ameliambia Pambazuko kwamba, “tunaweza kupima umakini wa mtu kwa kuangalia kinachomtoka mdomoni mwake, kwani, maneno anayoyatamka yanatwambia anafikiria nini, kuhusu kitu gani na kwanini.”

Dkt. Anita anataka kuona Taifa likijiuliza na kujibu maswali yafuatayo, kati ya mengine; “kadiri utendaji wa bandari zetu unavyohusika, tuko wapi leo? Tunataka tuwe tumefika wapi miaka mitano au kumi ijayo? Kusudi tuweze kufika huko tunapaswa kupita uelekeo gani na kukwepa uelekeo upi na kwa nini? Katika safari yetu kupitia uelekeo huo tunapaswa kupitia barabara zipi na kukwepi baraba zipi na kwa nini?”

Sheikh Mkuu wa Tanzania Sheikh Abubakar Zubeir bin Ally, anaungana na viongozi wengine wakuu wa dini akiwamo Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Gervas Nyaisonga, Askofu Mkuu wa KKKT, Dkt. Fredrick Shoo, Katibu wa Bakwata, Sheikh Khamis Mattaka na Mkuu wa Shura ya Maimam, Sheikh Ponda Issa Ponda kuhimiza Watanzania kujadili jambo lolote kwa hoja na kuvumiliana ili kulinda tunu za taifa; umoja, amani na udugu.

## Mkutano wa CCM

## CCM wazungumzia Bandari

Viongozi wa juu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiongozwa na makamu mwenyekiti wake, Abdulrahman Kinana, jana waliwakusanya wananchi katika mikoa ya Singida na Dodoma wakati wa ziara za chama hicho kuwaelezea msimamo wao kuhusu uwekezaji wa bandari unaotarajiwa kufanywa na

Kampuni ya DP World kutoka Dubai.

Chama hicho tawala kinaamini kwamba mkataba huo ni mzuri na utakapoanza kutekelezwa, Tanzania itanufaika zaidi kwa kupata kodi, ajira kwa wananchi na ujuzi kwa watendaji wazawa watakaokuwa wakifanya kazi bandarini.



*Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo akihutubia wananchi jana katika viwanja vya Bombadier, Singida.*



*Makamu Mwenyekiti CCM, akiteta jambo na Adam Kimbisa, ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho Dodoma. (Picha zote na CCM)*



*Umami wa wafuasi, wanachama na wananchi wakiwasikiliza vionogizi wa CCM wakati wakihutubia*

## Mkutano wa Chadema

### Chadema wazungumzia Bandari

**C**HAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) jana kiliitisha mkutano wa hadhara katika Kiwanja cha Bulyaga, Temeke, Dar es Salaam, ambapo viongozi wakuu wa chama hicho, wakiongozwa na mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, walihutubia umati.

Lengo kubwa la mkutano huo lilikuwa kuzungumzia msimamo wa chama hicho kuhusu uwekezaji katika baadhi ya bandari za Tanzania unaotarajiwa kufanywa na kampuni kutoka Dubai ya DP World.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, John Heche akizungumza katika mkutano uliofanyika jana katika Uwanja wa Bulyaga, Temeke. (Picha zote na Chadema).



Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Nyasa na mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, Mchungaji Peter Msigwa akizungumza katika mkutano huo wa hadhara.



Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, Godbless Lema akizungumza katika mkutano huo.

## Afrika Magharibi

### Mali yakubali katiba mpya kutumika

**H**ATIMEYE kiongozi wa kijeshi wa Mali, Kanali Assimi Goita ametangaza kuanza kwa mchakato wa kupatikana kwa katiba mpya ya nchi hiyo kufuatia kura ya maoni mwezi uliopita.

Serikali ya Kijeshi ya Mali juzi – Jumamosi ya Julai 22, ilitangaza kuridhia kuwepo kwa katiba mpya katika gazeti rasmi la serikali.

Tangazo hilo la Kanali Goita limetokea siku moja baada ya Mahakama ya Kikatiba ya Mali kuidhinisha matokeo ya mwisho ya kura ya maoni kuhusu rasimu ya katiba.

Serikali ya kijeshi ya nchi hiyo hapo awali ilisema kupitisha katiba mpya kutafungua njia ya uchaguzi na kurejea kwa utawala wa kiraia.

Uchaguzi mkuu wa Mali ulitarajiwa kufanywa Februari 2022, lakini ukaahirishwa hadi Februari 2024.

Tangu kuchukua mamlaka katika mapinduzi ya Agosti 2020, jeshi la Mali limeshikilia kuwa katiba itakuwa muhimu katika kujenga upya nchi.

Katika kuthibitisha matokeo ya mwisho ya kura hiyo ya maoni, mahakama ilikataa maoni ya upinzani ya kutaka matokeo yafutiliwe mbali kwa madai ya “ukiukaji sheria na ukosefu wa upigaji kura katika maeneo kadhaa ya nchi.”

Mali ilishuhudia mapinduzi mawili yaliyofuatana katika miaka ya hivi karibuni, moja mnamo Agosti 2020 na nyingine Mei 2021.

TRT Afrika

### Ghorofa laua 12 Cameroon

**W**ATU kumi na mbili wamepoteza maisha jana na wengine zaidi ya 20 kujeruhiwa baada ya jengo la ghorofa kuporomoka katika Jiji la Douala ambalo ni kitovu cha kibiashara nchini Cameroon.

Jengo hilo la ghorofa nne wakati likiporomoka, liliangukia jengo jingine dogo na kuongeza madhara Jumapili asubuhi.

“Takwimu za majeruhi zinaweza kuwa kubwa zaidi. Wafanyakazi wa uokoaji, wakisaidiwa na wanajeshi wa Cameroon, bado wanachimbua mabaki ya kuta kuona endapo miili zaidi inaweza kupatikana,” amesema Samuel Dieudonne Ivaha Diboua, gavana wa eneo la Littoral.

Kikosi cha zima moto cha jeshi kimeamriwa kuungana na Shirika la Msalaba Mwekundu nchini humo na huduma nyingine za uokoaji, kutafuta manusura walionasa chini ya vifusi.

Mshutuko mkubwa kwa wakazi

Wakaazi wanaoishi katika Mtaa wa Ndogbon ambapo tukio hilo limetokea walisema wamepatwa na mshtuko.

“Tulisikia watu wakipiga kelele, na tulijitahidi kusaidia baadhi ya watu kutoka kwenye mabaki, lakini hatukuweza kufanya hivyo kwa kutumia majembe yetu,” amesema Gaspard Ndoppo, ambaye anaishi karibu na majengo yaliyoporomoka.

Kuporomoka kwa majengo hutokea mara kwa mara huko Douala, wakati mwingine kutokana na majanga ya asili kama vile maporomoko ya ardhi na nyakati nyingine kwa sababu ya ujenzi duni, wenyeji wamesema.

Baraza la Jiji la Douala kwa sasa linabomoa nyumba katika maeneo hatarishi yanayoathiriwa na mafuriko au maporomoko ya ardhi.

TRT Afrika





## Kumbukizi

# Wicken: Msaidizi wa Mwalimu Nyerere, aliyefanya makubwa

Na Anna Chiduo-MWANSASU

**M**AJUKUMU yote ya Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hayawezi kuelezwa – kwa ukamilifu wake, bila kutaja jina la aliyekuwa msaidizi wake, Joan Everlyn Wicken.

Ni Watanzania wachache wa kipindi hiki wanaojua kazi kubwa aliyofanya Mama Joan Wicken kumsaidia Mwalimu Nyerere tangu mwaka 1958 alipokuja nchini kutokana na ombi la Nyerere kwa Chama cha Leba (Labour Party) cha nchini Uingereza.

Ilikuwa hivi; wakati wa harakati za kutafuta Uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere akiwa kiongozi wa chama cha Tanganyika African National Union (TANU), alienda Uingereza kwa mwaliko wa Chama cha Leba.

Alipokuwa huko alitembelea Chuo cha Ruskin mjini Oxford kilichokuwa kikitoa mafunzo kwa watu wazima ambao hawakufanikiwa kuingia vyuo vikuu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uwezo mdogo kifedha.

Mwalimu Nyerere alivutiwa na utaratibu wa chuo hicho wa kutoa mafunzo kwa watu wazima hususan wanasiasa kupewa mafunzo ya ustawi wa jamii, siasa, uchumi na pia kuwapika katika misingi ya usawa na uzalendo. Mwalimu akataka chuo cha aina hiyo kianzishwe nchini Tanganyika.

Chama cha Leba kikakubali ombi la Mwalimu. Kikampatia vijana wa kike wawili mmoja akiwa Joan Wicken ambaye alikuwa akifanya kazi kwenye Chama cha Leba na baadaye kuwa Ofisa Msaidizi katika Jumuiya ya Madola kutoka chama hicho akiwa katibu kwenye kitengo cha “Africa Education Trust” ambako alihusika sana na wanasiasa wa nchi zilizokuwa



Joan Wicken akiwa na Mwalimu Nyerere

zikipigania Uhuru.

Wakati wa uhai wake Mama Wicken alipenda kusimulia jinsi ambavyo alipokuja Tanganyika, walikuwa wakisafiri na Mwalimu Nyerere ama na viongozi wengine wa TANU na Umoja wa Wanawake (UWT) kwenda mikoani kufanya mikutano ya kuwahamasisha wananchi kujiunga na TANU.

Katika mikutano hiyo Mama Wicken na mwenziwe walikuwa wakipewa nafasi kueleza (kupitia mkalimani) kazi iliyowaleta nchini ya kuanzisha chuo cha watu wazima cha kutoa mafunzo kwa lengo la kujenga uzalendo na usawa miongoni mwa wananchi.

Katika mikutano hiyo wananchi

## Kumbukizi

## Wicken: Msaidizi wa Mwalimu Nyerere, aliyefanya makubwa

*Inatoka Uk. 9*

walihamasika sana, waliweza kuchangia senti moja moja, mahindi, maharage, mbuzi, kondoo, kuku, mayai, na kadhalika. Vitu hivyo vilinadiwa na kupatikana fedha zilizosaidia ujenzi wa Chuo cha TANU kilichokuwa kimedhamiriwa na kuamuliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Chama mwaka 1958. Chuo hicho ni Chuo cha Kivukoni, kilichopo Kigamboni ambacho sasa kinaitwa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Mama Wicken alikuwa akisimulia jinsi walivyokabidhiwa yaliyokuwa mahame ya hoteli pale Kigamboni kilipo chuo hicho. Eneo lile lilikuwa limezungukwa na nyasi ndefu na vichaka. Kazi ya kwanza ilikuwa ni kufyeka. Kwa hiyo, waliungana na wananchi waliojitolea kulifanyia usafi eneo hilo. Hatimaye ujenzi ulianza na chuo kilikamilika na kufunguliwa rasmi Julai 29, 1961.

Kumbe, wakati wote huo Mwalimu Nyerere alikuwa akiona uchapakazi, uwezo na moyo alikuwa nao Mama Wicken kusaidia kazi za Chama cha TANU. Ujenzi wa Chuo cha Kivukoni ulipokamilika Mwalimu akamuomba Mama Wicken aendelee kubaki nchini awe msaidizi wake.

Kwa maana hiyo tangu nchi ipate Uhuru Mama Wicken alikuwa Msaidizi wa Mwalimu Nyerere - Ikulu na baadaye Ofisi ya Rais Mstaafu Mwalimu; kazi aliyoundelea kuifanya hadi mwisho wa maisha ya Mwalimu.

Ni kazi gani alizokuwa akifanya Mama Wicken? Pengine ninaweza kusema nyuma ya pazia la miaka yote ya uongozi wa Mwalimu Nyerere hadi mwisho, alikuwapo mtu muhimu sana aliyelitwa "shangazi" na watumishi wenziwe - Mama Joan Wicken.



*Joan Wicken akiwa na Mwalimu Nyerere*

Kazi yake moja ilikuwa kutayarisha barua alizokuwa akiandika Mwalimu kwa marais na viongozi wa nchi za nje. Lakini, kazi kubwa na mahususi ilikuwa kuandika hotuba zote za Mwalimu Nyerere kwa lugha ya Kiingereza.

Ilikuwa Mwalimu akihitaji kutayarisha hotuba kwa lugha ya Kiingereza alikuwa akiketi na Mama Wicken na kumweleza alichotaka kukisema na kumpa muda wa hotuba husika. Kwa maana nyingine alikuwa akimpa muhtasari wa mawazo aliyonayo aliyotaka yaingie kwenye hotuba.

Mama Wicken alikuwa akiandika kwa hatimkato (shorthand) aliyoyataka Mwalimu. Akirudi ofisini kwake aliandaa hotuba na hatimaye kumpelekea Mwalimu kwa masahihisho, marekebisho ya nyongeza ama kupunguza kama Mwalimu alivyoona inafaa.

Mama Wicken aliwahi kunieleza kwamba, mwanzo Mwalimu alikuwa akibadili sana kile alichokuwa akimpelekea. Lakini baada ya muda kupita akawa ameshajua mwelekeo wa mawazo ya Mwalimu na nini Mwalimu

## **Wicken: Msaidizi wa Mwalimu Nyerere, aliyefanya makubwa**

alikuwa akitaka kukisema kwenye hotuba zake mbalimbali.


Kwa hiyo, ilifika wakati alikuwa akiandika hotuba, Mwalimu alikuwa haoni cha kusahihisha, kuongeza ama kupunguza. Pale Ikulu Mama Wicken alikuwa wa kwanza kutumia kompyuta. Alikuwa na kompyuta yake aina ya "Amstrad" aliyoitumia kuchapa kazi za Mwalimu.

Wakati anaanza kazi Ikulu mama huyu alimwomba Mwalimu Nyerere amkubalie kuingia ofisini saa 3 asubuhi hadi saa 12 jioni au zaidi. Chakula chake mchana kilikuwa vipande viwili vya mkate, nyanya na tunda moja. Chai aliinywa wakati wote na alikuwa mvutaji mzuri wa sigara.

Tangu alipofika nchini mwaka 1958 hadi anaondoka kurudi kwao Uingereza alikuwa akiishi kwenye nyumba ya kupangisha, kwenye vibanda vya Jeshi la Wokovu, Kilwa Road. Alikuwa na chumba kimoja chenye sehemu ya kitanda, sebule, sehemu ya kupikia vyote mahali pamoja, kwa kiingereza kinaitwa "bedsitter".

Pamoja na cheo kikubwa alichokuwanacho alikataa kuishi kwenye nyumba kubwa za Serikali. Kwa usafiri wa kwenda kazini Ikulu, alianza kutumia baiskeli baadaye scooter na hatimaye kigari kidogo kikiitwa mini-moc alichoesha mwenyewe miaka yote hadi Mwalimu alipostaafu. Baadaye Mwalimu aliamuru apewe gari na dereva wa kumwendesha kutoka kwenye kampuni ya Co-cabs.

Mwaka 1994 aliporudi kwao kwa matatizo ya kiafya, alipelekewa hundi ya mafao yake na asante kwa kazi kubwa na nzuri aliyofanya nchini mwetu kwa uaminifu mkubwa kwa miaka 33. Mama Wicken alikataa kupokea hundi ile. Akataka irudishwe serikalini akisema



*Mwalimu Nyerere wakiwa na wasaidizi wake wa karibu Annar Cassum, kushoto na Joan Wicken*

Watanzania walikuwa wakizihitaji fedha hizo kwa maendeleo yao, kuliko alivyohitaji yeye. Alidhihirisha uumini wake wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea!

Mwalimu alipoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kusini mwaka 1989, alimpa Mama Wicken kazi ya kusimamia Ofisi ya Tume ya Kusini iliyoanzishwa na viongozi wa nchi za Kusini kuratibu matatizo yanayozikabili nchi hizo na kutoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana nayo na kuyatatua. Makao Makuu ya Tume hiyo yalikuwa Geneva chini ya kivuli cha Umoja wa Mataifa na ikawepo ofisi ndogo Dar es Salaam chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Tanzania kwa kuwa Mwalimu alikataa kwenda kuishi Geneva.

Mwaka 1994 hali ya Mama Wicken kiafya ilipoanza kuzorota aliamua kurudi kwao Uingereza. Lakini, Mwalimu alimkumbusha kwamba hata akiwa huko kwao, bado alikuwa akimhitaji na ataendelea kuwa Msaidizi wake hadi kifo. Mama Wicken aliendelea

## Kumbukizi

## Wicken: Msaidizi wa Mwalimu Nyerere, aliyefanya makubwa

*Inatoka Uk. 11*

kuwa Msaidizi wa Mwalimu Nyerere kipindi chote kilichosalia cha maisha ya Mwalimu akikutana naye Geneva, Uswisi na kufanya naye kazi kila Mwalimu alipokwenda huko kikazi.

Wakati mmoja nilipata bahati ya kumtembelea Mama Wicken mjini Keighley alikokuwa akiishi na marafiki zake wa tangu shule, Bwana Mike na Bibi Maureen Yaffey. Aliniambia anasikitika hawezi tena kuandika vizuri hotuba za Mwalimu kwa sababu alikuwa hapati fursa ya kuongea na kubadilishana mawazo na Mwalimu kila siku kama ilivyokuwa alipokuwa nchini.

Mama Wicken alikuwa amejitokea utaratibu wake wa kwenda Msasani nyumbani kwa Mwalimu jioni kila siku ya kazi. Aliongea na Mwalimu kwa saa moja na zaidi na kupata mawazo ya Mwalimu kuhusu mambo ya kitaifa na kimataifa. Pia, kila akiongea na Mwalimu alikuwa akiandika maongezi yao kwa hatimkato.

Aliporudi kwao alianza kutafsiri maandishi hayo kutoka kwenye hatimkato kwenda kwenye maandishi ya kawaida. Ilikuwa ni kazi kubwa kwa sababu maandishi hayo yalijumu matukio na mazungumzo yake na Mwalimu tangu mwaka 1958 hadi kifo cha Mwalimu Oktoba 1999.

Kazi hiyo aliendelea nayo hadi kifo chake. Aliandika kwenye wosia wake kwamba yale yote yaliyomo kwenye maandishi hayo yasilolewe kwa yeyote hadi ipite miaka 30 baada ya kifo chake.

Utumishi uliotukuka wa Mama Wicken unapaswa kuenziwa sana. Alitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Chuo cha Kivukoni. Alisononeka chuo hicho kilipobadilishwa madhumuni yake ya kuwa chuo cha kuwapatia elimu watu

wazima na kuwapiga msasa viongozi wa Chama cha TANU na baadaye CCM, kikawa Chuo Kikuu cha kila mtu!

Mchango wake katika uanzishwaji wa Chuo cha Kivukoni unapaswa kuwekwa wazi kabisa kwa kumbukumbu na kwa faida ya vizazi vijavyo.

Joan Everlyn Wicken alitoka kwenye familia ya kawaida nchini Uingereza. Alizaliwa 12-7-1925. Mama yake alifariki Joan akingali mdogo. Alilelewa na baba yake ambaye alikuwa mwanaharakati wa vyama vya ushirika.

Kutokana na hali ngumu alikataisha masomo na kufanya kazi kwenye gereji. Alijifunza kupiga chapa na hatimkato (shorthand). Aliingia jeshini kwa kujitolea wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Baada ya vita alijiunga chuo kikuu na kupata digrii ya filozofia, siasa na uchumi.

Mama Wicken hakuwahi kuolewa, bali aliwahi kupata mchumba Mwafrika aliyekuwa kiongozi wa kisiasa nchini Kenya. Bahati mbaya kiongozi huyo aliuawa na kumwacha Mama Wicken na majonzi makubwa na hakutaka tena kuolewa.

Hata hivyo, alitokea kumpenda sana Kanali mmoja Mtanzania (jina nalihifadhi) aliyewahi kuwa mkuu wa mikoa mbalimbali kipindi cha uongozi wa Mwalimu Nyerere.

Mama Wicken hakuwa muumini wa dini yoyote, kwa Kiingereza alikuwa "earthiest".

Mwenyezi Mungu aendelee kuilaza roho ya Mama Wicken mahali pema peponi. Amen.

*• Mwandishi wa kumbukizi hii amekuwa Katibu Muhtasi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kwa miaka mingi. Anaishi Dar es Salaam.*



***Kunywa maziwa,  
imarisha afya***



**M**aziwa ya ng'ombe na mbuzi yamethibitika kuwa na mnyumbuliko wa vitamini, protini, mafuta, madini na maji; vitu ambavyo vinahitajika zaidi katika mwili wa binadamu kustawi.

Mazoea ya kunywa maziwa ni nguzo muhimu ya kumsaidia binadamu kuwa na afya bora, kupambana na baadhi ya magonjwa na kumpa kinga inayohitajika katika mwili.

Ni kutokana na ukweli huo, Kitonga Farm imeamua kusogeza karibu huduma ya kusambaza maziwa kwa wananchi.

Sasa maziwa hayo, pamoja na bidhaa zake zingine zinapatikana Bunju, Barabara ya Mbweni – kama unaelekea Shule ya Moga, Dar es Salaam.

Huduma hii ya maziwa pia mteja anaweza kuletewa hadi nyumbani endapo anaishi maeneo ya Bunju na Mbweni.

Njoo Kitonga House of Milk kwa kupata maziwa halisi ya ng'ombe na mbuzi kwa kuimarisha afya yako na familia.

Wasiliana nasi kwa namba ya simu:  
0748 109 109

Afya bora ndiyo mtaji  
mkubwa katika maisha.

***Chagua Kitonga Farm, Chagua Afya Njema.***

## Ethiopia

## Tigray sasa shwari, wawekezaji waitwa

**H**ALI ya utulivu na kuwepo kwa dalili za amani nchini Ethiopia, imeanza kuwapa faraja wawekezaji kutoka nje ya nchi hiyo, hasa wale wa madini kutangaza kurejea katika maeneo waliyowekeza kuendelea na shughuli zao.

Tayari kampuni ambazo zlikuwa zikijishughulisha na utafiti na uzalishaji wa madini huko Tigray zimeanza kurejea eneo hilo kuendelea na kazi zao.

Wizara ya Madini nchini Ethiopia imetangaza kuweka mikakati ya kurejesha shughuli za kuzalisha madini katika eneo la Tigray hivi karibuni ili kuwezesha kampuni ambazo zimekuwa zikifanya utafiti na kuchimba madini mbalimbali yakiwemo dhahabu katika eneo la Tigray, kuendelea na kazi zao.

Waziri wa Madini Million Mathews amefafanua kuwa hapo awali kampuni za kimataifa zilizokuwa zikiendesha uchunguzi na uchimbaji madini katika eneo hilo la Tigray, zimekuwa zikipata shida katika utekelezaji kazi zao kutokana na changamoto za awali.

Hata hivyo, Mathews amesema kuwa baadhi ya shughuli za uchimbaji zinaweza kuanza kazi sasa.

Mathews ameeleza kuwa mkataba wa amani wa Pretoria uliosainiwa mwaka jana baina ya Serikali ya Ethiopia na waasi wa TPLF, ili kusitisha mapigano, na kuleta amani ya kudumu, umeleta nafuu kwa wadau husika na sekta ya madini nchini humo kwa jumla.

Utulivu wa kudumu, umefanikisha mazingira mazuri iliyosababisha kampuni zinazyoshiriki katika uzalishaji na utafutaji wa dhahabu, saruji na madini mengine katika eneo la Tigray kurejea kazini.

Waziri huyo aliongeza kuwa tayari Kiwanda cha Saruji cha Mesbo kilichopo Tigray kimeanza kufanya kazi huku akiongeza kuwa kampuni zingine tayari zimeanza harakati za kurejea kuanza kazi.

Mathews ametaja kuwa tayari Benki ya Dhahabu iliyofungwa, imefunguliwa



Waziri wa Madini wa Ethiopia Million Mathews

tena na wataalamu wamepeva kibali cha kuanza ununuzi wa dhahabu huku akiongeza kuwa wanashirikiana na utawala wa mpito wa Ukanda wa Tigray ili kufufua uwezo wa uzalishaji wa sekta hiyo.

Waziri huyo wa nchi pia alisema uongozi mpya wa mpito wa Tigray umewachukulia hatua kali waliokuwa wakiingia na kuzalisha madini kiholela kinyume cha sheria.

Mathews amesifu kuwa hatua hii itawawezesha wachimbaji halali wenye leseni na vyama vya uchunguzi kuanza kufanya kazi kwa kujiamini.

Aidha, imeripotiwa kuwa kampuni nyingine za kimataifa za uchimbaji madini, ikiwa ni pamoja Newmont, maarufu katika sekta ya madini ya dhahabu duniani, zimethibitisha kuwa yataanza tena shughuli zao katika eneo hilo hivi karibuni.

Waziri huyo amesema kuwa serikali iko tayari kutoa msaada wowote ili shughuli za utafiti, uchimbaji na hata nbiashara ya madini yoyote isikwame.

Amesema Ethiopia kwa sasa inahitaji kodi kutoka kwenye madini ili kuweza kuhudumia wananchi kwa ujenzi wa miundombinu, hospitali, kununua dawa na kuagiza bidhaa kutoka nje.

## *Tangaza na* **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au Barua-  
Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Fukuto la Bandari

### TLS yahadhari, yatoa ushauri

**C**HAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimefanya mapitio, kuchambua na kutoa maoni yake juu ya mkataba wa serikali kwa serikali (IGA) ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirati ya Dubai umefungwa.

Mkataba huo wa ushirikiano, umejikita zaidi katika uendeshaji wa bandari za Tanzania, ambapo kampuni ya DP World ya Dubai, itakuwa na jukumu la kuendesha na kusimamia baadhi ya bandari za bahari na maziwa ya Tanzania.

TLS inatambua na inakubali juhudi nzuri za serikali za kuwavutia wawekezaji wa kigeni na kuchochea uchumi wa taifa kwa faida ya ustawi wa nchi.

Mawakili hao katika tamko lao, wameeleza kwamba wanaunga mkono juhudi zinazoboresha ustawi wa taifa, utawala wa sheria.

Walakini, TLS inasihii Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha ushiriki wa umma wa kutosha na kwa kina katika hatua za kupanga, kujadili, na kufanya uamuzi kuhusu rasilimali za taifa na uwekezaji wa aina hiyo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haswa Ibara 8 na 9, na haswa, Ibara 21 (2), ambayo inampa kila raia haki na uhuru wa kushiriki kikamilifu katika mchakato unaosababisha uamuzi juu ya masuala yanayomhusu yeye, ustawi wake au taifa.

TLS inaona kuwa Mkataba wa Serikali kwa Serikali (IGA) haukufanyiwa kazi vizuri, kusababisha utata, shaka, utata na tafsiri tofauti na wahusika tofauti.

Wiki iliyopita, gazeti hili la Pambazuko lilianza kuchapisha mtazamo wa TLS kuhusu kuwepo kwa vipengele ama vifungu vinavyopuuzwa maslahi mapana ya taifa na kutoa mapensekezo, ifuatayo ni sehemu ya mwisho ya mtazamo na ushauri wa wanasheria hao;

2.7.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Upeo wa Kifungu cha 27 haupokelezi kwa sababu unapanua wajibu kwa HGAs na Mkataba wa Mradi wa baadaye. Hii



Rais wa TLS Halord Sungusia

inaleta masuala kwa sababu inawezekana kuifanya Tanzania iwe na dhima kwa uvunjaji usio wa makusudi wa Kifungu cha 27.

HGAs na Mkataba wa Mradi utajumuisha vifungu vinavyoshughulikia kutokuwa na mgogoro. Hakuna haja ya kuongeza wajibu wa kutokuwa na mgogoro kwa HGAs na Mkataba wa Mradi. Sura ya 1 ya Mkataba wa Haki na Wajibu wa Kiuchumi wa Nchi inaeleza kanuni za uhusiano wa kiuchumi wa kimataifa.

Mkataba unalazimisha kwamba uhusiano wa kiuchumi, kisiasa, na vinginevyo kati ya Nchi unapaswa kusimamiwa, miongoni mwa mambo mengine, na kanuni zifuatazo: (a) Uzalendo, utii wa eneo, na uhuru wa kisiasa wa Nchi. Kuifanya Jamhuri ya Muungano iwe na hali ya kisheria ya hali ya baadaye ni isiyo ya kawaida na inaweza kuhatarisha uhuru wa kiuchumi ulioelezwa katika Mkataba.

2.7.5. Athari Inayotarajiwa ya Shida kwa Nchi Yetu:

Nchi inalazimishwa mapema kuwakilisha na kuhakikisha kwamba baada ya HGAs na Mkataba wa Mradi



## Fukuto la Bandari

### **TLS yahadhari, yatoa ushauri**

**Inatoka Uk. 17**

kuanza kutumika, ambao masharti na masharti yake bado hayajakamilishwa na kutekelezwa, haitashiriki katika makubaliano yoyote ya ndani au ya kimataifa au majukumu, au kuwa na wajibu wa kisheria wa kuzingatia au kutekeleza sheria, kanuni, au makubaliano ya ndani au ya kimataifa, ambayo yanapingana au kuanzisha au kutekeleza Mkataba husika au HGA husika na Mkataba wowote wa Mradi ambao Nchi Mshiriki huyo ni mshiriki.

2.8 – Uwezo wan chi za mkataba na watia saini wao

2.8.1. Kifungu cha 28 cha IGA kinabainisha uwezo wa nchi za mkataba na watia saini wao.

2.8.2. Uchunguzi wa TLS:

TLS imebaini kasoro kadhaa katika kifungu hiki. Kichwa cha kifungu kinahusu nchi za mkataba. Hii, kwa mujibu wa sheria za kimataifa, hasa GA Res. 3281(xxix), UN GAOR, 29th Sess., Supp. No. 31 (1974) 50 Mkataba wa Monte Video wa 1933, kinabainisha ufafanuzi wa nchi. TLS inaamini kwamba kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mtiwa Saini ana uwezo wa kisheria wa kusaini mkataba kama nchi



**Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Jaji Dkt.  
Eliezer Feleshi**

ya mkataba.

Hata hivyo, TLS imebaini kwamba taasisi mbalimbali zimeelezea wasiwasi wao kuhusu hadhi ya kisheria ya Emirate ya Dubai. TLS haiwezi kutoa maoni yake kuhusu hadhi ya Emirate ya Dubai hadi itakapopata maoni ya kisheria kutoka kwa taasisi yenye ujuzi wa Dubai.

Maoni kama hayo yanapaswa kufafanua masuala kama vile ikiwa Emirate ya Dubai inakidhi vigezo vya kuwa nchi kwa mujibu wa sheria za kimataifa au iko chini ya Umoja wa Falme za Kiarabu; ikiwa kumbukumbu za nchi za mkataba ni sahihi au la; ikiwa kumbukumbu ya utangulizi kuhusu Emirate ya Dubai kama nchi ya mkataba ni sahihi kisheria; ikiwa mtiwa saini kwa niaba ya Emirate ya Dubai anaweza kuifunga nchi kwa mkataba wa kimataifa na ikiwa utengenezaji wa jina na cheo cha shahidi wa wakala wa Dubai ni sahihi. Kwa sasa, TLS haiwezi kutoa maoni yake kwa uhakika kuhusu kuzingatia kwa masharti ya Kifungu cha 28.

2.8.3. Mapendekezo ya TLS:

TLS inaamini kwamba ikiwa kuna shaka yoyote kuhusu Kifungu cha 28 cha IGA, maoni ya kisheria tofauti yanapaswa kupatikana kutoka kwa taasisi ya Dubai yenye ujuzi wa sheria za Dubai.

2.8.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS:

Mapendekezo ya TLS yanatokana na ukweli kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina mamlaka kwa mujibu wa Kifungu cha 63(3)(e) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuidhinisha mikataba ya kimataifa inayohitaji idhini.

2.8.5. Athari Inayotarajiwa ya Masuala kwa Nchi Yetu:

Isipokuwa masuala yaliyotajwa hapo juu yatatatuliwa kwa kitaalamu katika hatua za awali, hadhi ya kisheria na uwezo wa kufunga mkataba huu wa Serikali kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirate ya Dubai inaweza kuwa suala la mzozo wa baadaye chini ya

**Fukuto la Bandari****TLS yahadhari, yatoa ushauri***Inatoka Uk. 17*

sheria za kimataifa.

**2.9 – Kifungu cha utulivu**

2.9.1. Kifungu: Kifungu cha 30 kinabainisha kwamba Tanzania itatekeleza marekebisho ya kisheria yanayohitajika kuimarisha mazingira mazuri ya uwekezaji.

Vyama vinakubaliana kwamba mfumo wa kisheria na mkataba unaohusiana na Mradi utaendelea kudumishwa kwa njia inayofanana na kuridhisha kwa pande zote, Kampuni ya Mradi, na kwamba maelezo ya kuridhika hayo yatakubaliwa kati ya DPW na TPA na yataonyeshwa katika HGAs.

**2.9.2. Uchunguzi wa TLS:**

TLS inazingatia kwamba kifungu hiki, kinachohitaji kuboreshwa kwa miundombinu ya kisheria ya uwekezaji wa Tanzania, kinaweza kuwa na athari chanya kwa Tanzania. Hata hivyo, TLS ina wasiwasi juu ya maneno ya Kifungu ambacho kinahitaji Mradi uwe imara kwa njia inayofanana na kuridhisha kwa pande na Kampuni ya Mradi.

Pia inajulikana sana kuwa mazingira ya kisheria yaliyopo katika sekta zote hayafai kwa uwekezaji wa kibinafsi au PPP ikiwa ni pamoja na sheria ya PPP Biashara nyingi zinaendeshwa kwa msingi wa dhamira ya uongozi wa kisiasa wa kuboresha hali ya uwekezaji. TLS inaona kwamba sera ya uwekezaji haijabadilishwa, lakini kilichobadilika ni sheria ambazo zinazuia uwekezaji.

Sheria hizi kwa kiasi kikubwa zinaendelea kuwepo. Ndio maana uongozi wa TLS, wakati wa ziara ya heshima kwa Rais (Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan) mwaka 2021, ulipendekeza kwamba marekebisho kamili ya mfumo wa kisheria na udhibiti unaathiri uwekezaji, ikiwa ni pamoja na mfumo wa haki ya jinai, uwekewe kipaumbele.

Mbinu ya kipande-kwa-kipande haiwezi kuruhusu ushiriki wa wadau katika mageuzi. Zaidi ya hayo, TLS



**Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamisi wa Bandari Placidius Mbossa**

inatambua Kifungu cha Utulivu katika IGA, HGA, na mikataba mingine ya uwekezaji wa kimataifa kama njia ya wawekezaji wa kigeni kupunguza au kusimamia hatari za kisiasa zinazohusiana na miradi yao, na kwa Nchi Mwenyeji kuwavutia wawekezaji.

TLS pia inatambua aina mbalimbali za kifungu cha utulivu, kikiwemo kifungu cha kufungia, kifungu cha usawa wa kiuchumi, na kifungu cha hybrid. IGA ya sasa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirates ya Dubai imechagua kifungu cha kufungia.

Hata hivyo, TLS inaamini kwamba kifungu cha hybrid kingekuwa bora na faida kwa watu wa Tanzania, kutoa makubaliano yenye usawa kati ya pande mbili. TLS pia ilibaini kwamba kifungu

## **TLS yahadhari, yatoa ushauri**

*Inatoka Uk. 18*

cha Utulivu chini ya Kifungu kilikuwa wazi bila kuwa na kikomo kwa masharti ya kifedha au wakati maalum. TLS inaamini kwamba kifungu cha utulivu kischokuwa na kikomo kinaweza kuwa na athari kubwa kwa sera na utawala wa kodi wa nchi yetu baadaye.

### **2.9.3. Mapendekezo ya TLS:**

TLS inapendekeza kwamba Kifungu cha 30 kirekebishwe ili kuondoa utata wa tafsiri ambao unaweza kusababisha migogoro ya baadaye. TLS pia inapendekeza kwamba serikali ifanye mageuzi kamili ya kisheria na udhibiti kwa sekta kwa sekta, kwa kuchukua mafundisho kutoka kwa Programu ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara kwa Tanzania (BEST).

Katika muktadha huu, Kifungu cha 30 kinapaswa kurekebishwa ili kuingiza kifungu cha utulivu cha hybrid. Matumizi ya kifungu cha utulivu yanapaswa kuzingatia masharti maalum ya kifedha na wakati maalum ili kupunguza athari yake kwa sera na utawala wetu wa kodi.

### **2.9.4. Sababu za Mapendekezo:**

Aina hatari zaidi ya kifungu cha utulivu ni kifungu cha kufungia, ambacho lengo lake ni kufungia sheria inayohusiana na uwekezaji kwa muda mrefu kama leseni inaendelea.

Kama matokeo, hakuna kifungu katika mkataba wa IGA wa sasa kinachoweza kuzidiwa na zoezi la haki za serikali bila idhini ya wazi ya mwekezaji. Aina nyingine za kifungu cha utulivu ni pamoja na kifungu cha usawa wa kiuchumi na kifungu cha kihybrid ambacho lengo lake ni kudumisha usawa wa kiuchumi kati ya pande wakati wa kusaini mkataba.

Haki zinazotokana na kifungu cha utulivu mara nyingi hutekelezwa na mahakama katika usuluhishi wa uwekezaji-nchi, mara nyingi ikisababisha kupatikana kwa uvunjaji na kuongoza kwa wajibu wa nchi mwenyeji kulipa fidia kwa mwekezaji.

2.9.5. Madhara Yanayowezekana kwa Nchi Yetu: Kifungu cha kufungia



*Wasiri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa*

kinaweza kuzuia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza hatua muhimu za kulinda haki za wananchi na kutekeleza sheria za kitaifa zinazotumika mahali pengine nchini.

Matibabu ya upendeleo yanaweza kuzuia ushindani na kuwakatisha tamaa wawekezaji wa ndani. Kifungu cha utulivu, haswa kifungu cha kufungia na kifungu cha usawa wa kiuchumi, kinakosolewa na Amnesty International kwa sababu kinawapa wawekezaji wa kigeni na miradi yao msamaha kutoka kwa kuzingatia sheria za haki za binadamu.

### **3. Hitimisho**

Kwa kumalizia, TLS itaendelea kufuatilia utekezaji wa mapendekezo yake ili kutoa msingi kwa kuingilia kati kwa siku zijazo kama itaonekana kuwa sawa na muhimu.

TLS ina matarajio ya kweli kwamba mapendekezo haya yatapata tahadhari inayofaa kutoka kwa mamlaka husika. Tunasisitiza ahadi yetu ya kusaidia katika kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa taifa lenye mafanikio ambapo kila mtu anapewa uhuru, haki, udugu, na amani.

## MANDONGA 'CHALI...'



Bondia maarufu wa Tanzania, Karim Mandonga (Mzee wa Sugunyo), amepata pigo lake la kwanza nchini Kenya baada ya mpinzani wake, Daniel Wanyonyi almaarufu 'Mwanawefwe' kumlambisha 'sakafu' mara mbili katika pambano lililokuwa la kuwania mkanda lililofanyika Jiji la Nairobi Jumamosi iliyopita. Wanyonyi hata hivyo alishinda kwa pointi. Pambano la awali la mahasimu hao lilifanyika Januari mwaka huu, ambapo Mandonga alimchakaza Wanyonyi. Picha na Ultrafight

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

